JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YAWILAYAYA MPWAPWA
SHULE YA SEKONDARI MPWAPWA

S.L.P 03,
MPWAPWA
29 MACHI, 2022.

Simu ya Ofisini: 026 - 2324 074

Simu ya Mkononi;

0787-714334 – MKUU WA SHULE.
0786-649031/0629-806043 –MAKAMU MKUU WA SHULE.
0713-596955/0766-554114 –OFISI YA TAALUMA.
Email: mpwapwasec@gmail.com

KUMB.NA. MPW/SS/AL/JI/14/2022.

Kwa Mzazi wa: ……..
…….

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO JULAI, MWAKA 2022 SHULE YA SEKONDARI MPWAPWA.

Napenda kukuarifu kuwa kijana/binti yako amechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Mpwapwa Kidato cha tano mchepuo wa (Weka alama ya vema **(√)** katika mchepuo husika); **HGK (_), HKL (_), CBG (_) AU PCM (_),** Mwaka 2022. Nakupongeza sana kwa kijana wako kufaulu na hatimaye kupata bahati ya kuchaguliwa kujiunga na shule hii. Shule itafunguliwa tarehe **……../2022** na ndiyo siku ambayo kijana wako anatakiwa awe ameshafika shuleni.

A. MAHALI SHULE ILIPO:

Shule yetu ipo Mkoa wa **Dodoma**, Wilaya ya **Mpwapwa**, kata ya **Mpwapwa** mjini. Mji wa Mpwapwa unafikika kwa mabasi ya moja kwa moja kutoka Dodoma. Upo usafiri wa kila siku wa mabasi kutoka Dodoma ambayo hufanya safari zake kuanzia saa 03:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni. Usipopata usafiri wa aina hii unaweza kupanda mabasi yanayoelekea Gairo, Morogoro au Dar Es Salaam na kushuka kituo cha ***Mbande***, mahali ambapo ni njia panda ya kuelekea Mpwapwa na Kongwa. Tafadhali sana usipande gari au basi linaloekea Kongwa, subiri linaloelekea Mpwapwa.

Endapo unatokea Dar-es-Salaam au Morogoro unashauriwa kutumia basi lolote kati ya mabasi yanayofanya safari zake kuja Mpwapwa moja kwa moja; usafiri huu upo kila siku. Ukikosa basi la moja kwa moja tumia basi lolote linaloelekea Dodoma na uteremkie Mbande na kupata usafiri wowote unaolekea Mpwapwa. Unatahadharishwa tena kutotumia magari yanayoishia Kongwa.

Kwa wale watakaotumia usafiri wa treni, tunashauri kuteremkia Dodoma mjini ambapo ni rahisi kupata usafiri wa kuelekea Mpwapwa Mjini moja kwa moja. Mabasi yanayokuja mpwapwa huanzia safari zake Dodoma Mjini kwenye kituo kiitwacho ***Soko la Ndugai lililopo karibu na stendi kuu ya mkoa eneo la Nanenane.*** Unapokaribia Shule ya Sekondari Mpwapwa teremkia kituo kiitwacho ***Ujenzi*** ambacho ni mita 40 tu kufika lango kuu la kuingilia shuleni (usipande boda boda, tembea kwa miguu). Ukiingia ndani ya eneo la shule, upande wako wa kushoto utaona

Jengo la Utawala (Administration Block), Ukumbi wa Shule na Ofisi za Walimu, hapo utakuwa umefika Shule ya Sekondari Mpwapwa. Ukiwa umetimiza maagizo yaliyoko kwenye barua hii mtoto wako atapokelewa Ofisi ya Makamu mkuu wa shule. Mwanafunzi atapokelewa rasmi pale atakapokuwa ametimiza yafuatayo:

B. MICHANGO MBALIMBALI;

- **MUHULA WA KWANZA**

01. Ada ya shule kwa muhula.....Tshs35,000/=
02. Fedha yatahadhari (hairudishwi)..... Tshs 5,000/=
03. Kukodi godoro kwa muhula.....Tshs 10,000/=
04. Mchango wa Taaluma kwa muhula… .....Tshs15,000/=
05. Mchango wa Mlinzi na Wapishi kwa muhula… .Tshs15,000/=
06. Ukarabati wa samani kwa mwaka..... Tshs22,000/=
07. Kitambulisho ..... Tshs 6,000/=
08. Mchango wa kuzibua vyoo na maji taka kwa mwaka.....Tshs.5,000/=

JUMLA KWA MUHULA WA KWANZA (HGK, HKL, PCM na CBG):…….Tshs.113,000/=

- **MUHULA WA PILI**

1. Ada ya shule kwa muhula.....Tshs35,000/=
2. Kukodi godoro kwa muhula.....Tshs 10,000/=
3. Mchango wa Taaluma kwa muhula… .....Tshs15,000/=
4. Mchango wa Mlinzi na Wapishi kwa muhula… .Tshs15,000/=

JUMLA KWA MUHULA WA PILI (HGK, HKL, PCM na CBG):……..….Tshs.75,000/=

JUMLA KUU KWA MWAKA=188,000/=

- Fedha zote ziwekwe katika akaunti namba: **NMB 50401200041(MPWAPWA SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTION)**

Akaunti hiyo ni ya NMB. Andika jina la mwanafunzi kwenye bank- pay inslip na kuja nayo shuleni (bank – pay – inslip original tu ndiyo itapokelewa shuleni na siyo photocopy)

C. TAALUMA:

Katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaendeleza ufaulu waliokuja nao hapa shuleni kila mwanafunzi anatakiwa kufaulu vizuri kila somo kwa ***kiwango kisichopungua alama 60***. Endapo atashindwa kufikia alama hizo katika mitihani au majaribio mawili mfululizo itabidi mzazi au mlezi uliyeandikishwa uje shuleni kushauriana na uongozi wa shule njia sahihi ya kumsaidia kijana wako.

Mwanafunzi anatakiwa kuja na orodha ya vitabu vilivyoorodheshwa katika kiambatanisho A iliyowekwa katika ukurasa wa mwisho wa fomu hii. Kwa somo la **GENERAL STUDIES** (wanafunzi wote) na BASIC APPLIED MATHEMATICS (**BAM**) **LAZIMA** kila mwanafunzi aje na kitabu kimojawapo kati ya vilivyoorozeshwa katika masomo hayo. Kwa masomo mama ya mchepuo kila mwanafunzi aje na angalau **VITABU VIWILI (2)** au vyote kwa kadri ya uwezo wa mzazi na vitabu vingine mzazi ataendelea kununua kidogokidogo kama hataweza kumudu kuvinunua vyote kwa wakati mmoja kwani vyote vilivyoainishwa na walimu wa masomo ni muhimu. Lengo kuu la kuainisha vitabu hivyo ni kwaajili ya maendeleo ya kitaaluma ya mwanafunzi katika kufikia malengo yake kitaaluma.

D. VIFAA VYA KUJA NAVYO:

01. Bunda moja la karatasi ya Photocopy (A4) kwa kila muhula kwa ajili ya matumizi ya mazoezi na mitihani. Wanafunzi wanaojiunga kwa mchepuo wa **PCM na CBG** waje na Scientific Calculator, HKL waje pia na Oxford Advanced Learners Dictionary.
02. Picha 04 (**nne**) za **"Passport size"** kwa matumizi ya ofisi.
03. Raba, bukta na, T-Shirt 2 za rangi nyekundu mpya **(zisiwe na maandishi ama nembo yoyote)** kwa ajili ya michezo.
04. Kalamu na Daftari za kutosha kulingana na masomo yaliyo kwenye mchepuo aliochaguliwa pamoja na somo la **General Studies** (kwa wote) na Basic Applied Mathematics **(BAM)** kwa tahasusi ya **CBG**.

05. Vifaa vya usafi vya kuja navyo **(kwa mwaka**):
    - Mchepuo wa CBG na PCM walete Kwanja/Fyekeo-01 na Jembe lenye mpini imara-01
    - Mchepuo wa HGK na HKL walete Reki-01, Kwanja/Fyekeo-01 na Hard Bloom (mfagio mgumu wa kusugulia sakafu)-01.
06. Tochi moja ya kusomea ya betri za kawaida ama ya kutumia nishati ya jua (solar) kwa ajili ya kusomea na kutumia wakati umeme unapokatika shuleni.
07. Ndoo **mbili** safi za lita 10 kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi shuleni **(tafadhali usirahisishe kwa kuja na ndoo kubwa ya lita 20, ndoo ziwe mbili za lita kumi kila moja)**

E. SARE YASHULE:

1. WAVULANA:

Mashati meupe mawili ya tetroni ya mikono mifupi mawili (2), suruali mbili (2) za heshima zenye marinda za rangi ya damu ya mzee (siyo za kubana na chini iwe na upana wa inchi 16 pia iwe na mkunjo wa chini)),viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba (vya kupigwa na rangi) na sweta la rangi ya damu ya mzee na tai ndefu ya damu ya mzee, koti la suti lenye rangi ya damu ya mzee (la kawaida lisilo na alama nyingine ama rangi nyingine ama nembo yoyote) na soksi nyeusi, j***acket haliruhusiwi kabisa.***

NB: Mwanafunzi anatakiwa kunyoa nywele **fupi**, saizi moja na sio mtindo wa panki ama kiduku lakini pia sio **kipara** (kutoa nywele zote kichwani).

2. WASICHANA:

Shati/blauzi nyeupe mbili za tetroni ya mikono mifupi, sketi mbili za heshima za rangi ya damu ya mzee zenye marinda makubwa yanayoelekea sehemu moja na zenye urefu unaofika kwenye kifundocha mguu, viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba (vya kupigwa kiwi) na sweta la rangi ya damu ya mzee na tai ndefu ya damu ya mzee, koti la suti lenye rangi ya damu ya mzee, soksi nyeupe.***Muislamu akiona inafaaa" Hijab" inaruhusiwa ambayo atavalia na sketi ndefu yenye marinda mpaka chini kwenye kifundo chamguu.jacketi haliruhusiwi kabisa***. **Na suruali kwa wasichana pia haziruhusiwi.**

NB: Mwanafunzi anatakiwa kunyoa nywele **fupi**, saizi moja na sio mtindo wa panki ama kiduku lakini pia sio **kipara** (kutoa nywele zote kichwani). Wasichana hawaruhusiwi kusuka nywele ama kuwa na nywele ndefu za kubana.

3. SARE BAADA YAMASOMO:

Baada ya masomo wavulana na wasichana wanatakiwa kuvaa sare maalumu (shamba dress); Wavulana watavaa suruali nyeusi za kitambaa zenye marinda-chini zenye upana wa inchi 16 na mkunjo wa chini (aje nazo mbili) zenye heshima na maadili ya kitanzania pamoja na tisheti nyekundu zenye kola na nembo ya shule. Wasichana nao watavaa sketi za Kijani ndefu kupita magoti zenye urefu unaofika kwenye kifundo cha mguu na tisheti nyekundu zenye kola na nembo ya shule. Wanafunzi wote (wavulana na wasichana) watatumia track suit ya rangi ya kijivu **isiyo na nembo ama maandishi makubwa na sweta la Truck suit lisiwe na kofia** wakati wa michezo au kazi za mikono. Shamba dress pia zitavaliwa hata usiku wakati wa maandalizi ya jioni pamoja na koti za truck suit za kijivu kuijikinga na baridi usiku.

NB:

1. **Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa shuleni hivyo mwanafunzi siku ya kuripoti aje akiwa amevaa sare kamili ya shule**
2. **Ili kuwa na sare moja inayofanana kwa wanafunzi wote na sisi walezi kurahisisha suala letu la malezi T-shirts za shule (shamba dress) zinapatikana hapa hapa Mpwapwa Mjini kwa ndugu Sisty Karia wa namba – 0784427439.**

4. VIFAA VINGINE: Vifaa vingine ni kamaifuatavyo:

i. Shuka mbili rangi ya sky bluu au
   rangi. ya pink, Mto kwa ajili ya kulalia.
ii. Sanduku (trunk) imara la kuhifadhia mali yake kwa usala mabwenini.
iii. Seti ya vyombo safi vya chakula: sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
iv. Galoni au chombo kidogo cha kuhifadhia maji yakunywa.
v. Fedha kiasi (Pocket money) cha uwezo wako kwaajili ya matibabu yake mwenyewe kwenye hospitali ya Wilaya ambayo iko karibu na shule (inapakana nashule).
vi. Neti kwa ajili ya kujikinga na mbu
vii. Blanketi moja kwa ajili ya kujikinga na baridi.

F. MATIBABU:
Hospitali ya Wilaya ipo jirani kabisa na shule ambako huduma za afya hutolewa kwa kuchangia gharama fulani au kwa kutumia Kadi ya Bima ya Afya (NHIF). Kwa mzazi au mlezi ambaye hujamkatia bima kijana wako unatakiwa kumpatia fedha kwa ajili ya matibabu au fedha ya kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (**CHF**) ambayo ni **Tshs 5,000/=** kwa mwaka ambapo shule itafanya utaratibu wa kuunda kaya ya watoto sita kwa mujibu wa maelekezo ya serikali, ili aweze kupata kadi ya **CHF** itakayodumu kwa mwaka mmoja tu.(Fedha hiyo ataikabidhi kwenye ofisi ya makamu mkuu wa shule).
NB: Kadi za **CHF** zinafanya kazi ndani ya mkoa mmoja tu, ambako Shule husika ipo.

G. Mwanafunzi **HARUHUSIWI KUMILIKI SIMU YA MKONONI**, **PASI YA UMEME**, **CAMERA** na **LAP TOP, REDIO ama kifaa kingine chochote cha kielektroniki hapa shuleni**.Tafadhali sana tena sana na kwa heshima kubwa mzazi/mlezi mwenzetu usimruhusu kijana wako kuja nayo simu ya mkononi kwa namna yeyote ile. Kumruhusu kuja nayo ni kumtafutia matatizo kama inavyojieleza katika sheria za shule ambazo nimekuletea mzazi ili uzisome na kuzijadili na kijana wako.

Mwanafunzi afike na barua hii pamoja na fomu ya kukubali kujiunga na Shule ya Sekondari Mpwapwa na cheti cha Daktari wa hospitali ya Serikali kuthibitisha afya yake (tafadhali usifiche kama mwanao ana tatizo fulani la kiafya) na Results slip ya kidato cha Nne. Vitu hivi pamoja na vingine alivyoagizwa atavionesha au kuvikabidhi wakati wa kuripoti Shuleni.

H. MAMBO MENGINE YA KUZINGATIA WAKATI WA KURIPOTI NA UKIWA SHULENI;

1. Tunatoa wito kwa mzazi/mlezi wa Mwanafunzi kuwa mtumie zaidi siku za kazi **(JUMATATU – IJUMAA** kuwaleta wanafunzi shuleni na kama utamleta siku za mwisho wa wiki (weekend) iwe ni kwa dharura tu na ufanye mawasiliano kwa kutumia namba tajwa hapo juu katika ukurasa wa kwanza wa fomu hii.

2. Siku ya kuripoti shuleni Mwanafunzi aje akiwa amevaa sare kamili ya shule na si vinginevyo.

3. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na mafuta ya kujipaka yenye harufu kali wala marashi ya aina yoyote ili kuwakinga wenzao wenye maradhi ya kifua cha kubana kama vile athma au mzio (allergies). Mwanafunzi aje na mafuta ya kujipaka ya kawaida, yasiyo na marashi wala harufu kali. Pia ni marufuku kuja na marashi (perfume) ya aina yoyote hapa shuleni na mwanafunzi atakayekutwa navyo atachukuliwa hatua kali na za kisheria.

4. Kila mwanafunzi ahakikishe **lazima** anakuja na kitabu kimojawapo kilichoorodheshwa katika kipengele cha taaluma kwa somo la **GENERAL STUDIES (GS) NA BASIC APPLIED MATHEMATICS (BAM) na angalau kitabu zaidi ya kimoja kwa kadri ya uwezo wa mzazi kwa masomo mama ya tahasusi aliyopangiwa**

5. Mawasiliano kati ya mwanafunzi na mzazi akiwa shuleni yafanyike nyakati za mapumziko yaani; Saa nne na dakika ishirini asubuhi **(10:20 am**) asubuhi mpaka saa tano kamili asubuhi **(11:00 am)** asubuhi na saa nane na dakika isihirini (**14:20 am) mchana** mpaka saa tisa na dakika arobaini alasiri **(15:40 pm**) kupitia walimu wa madarasa na matron kwa wanafunzi wa kike. Hata hivyo mzazi anaweza kupiga simu nje ya muda tajwa hapo juu kwa dharura tu, kwa mkuu wa shule ama makamu mkuu wa shule ama mwalimu wa malezi shuleni **(0787036185).** Pia wanafunzi wa kike wanaweza kutumia simu za walimu wa madarasa wakati wa mchana ila mara nyingi watatumia simu za matrons wa shule.

Pia kumekuwa hali ya wazazi kupigiwa simu na watu ambao hujitambulisha kama walimu wa shule ya sekondari mpwapwa na kutoa taarifa za uongo kwa wazazi/walezi kuwa mwanafunzi anaumwa na kudai fedha za matibabu. Tafadhali mzazi/mlezi kabla ya kufanya maamuzi yoyote yale piga simu shuleni kujiridhisha na taarifa hizo.

Karibu Sana Shule ya Sekondari Mpwapwa

OMARI T. OMARI
MKUU WA SHULE
0787 – 714 334

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI MPWAPWA

Shule ya Sekondari Mpwapwa inaendeshwa kwamujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 yamwaka 1978 pamoja na marekebisho yake. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Kijana anatakiwa kuzingatia mambo yamsingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- Heshima kwa viongozi, wazazi/walezi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa jumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu nalazima.
- Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni (NightPreparation)
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezoutakazopewa.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shulehii.
- Kutunza usafi wa mwili pamoja na mazingira ya shule kwajumla.
- Kuvaa vizuri huku ukiwa umechomekea sare ya shule wakatiwote.
- Kuzingatia ratiba yote ya shule wakati wote kuanzia asubuhi wakati wa kuamka hadi usiku wakati wa kwendakulala.
- Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kunywa pombe,kuvuta sigara, kufuga kucha na nywelendefu.
- Ni lazima mwanafunzi aheshimu na kukubali tofauti za ki dini, ki utamaduni na siasa zilizomo katika jumuiyayetu.

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kijana kufukuzwa shule:

01. Wizi
02. Uasherati naushoga
03. Ubakaji
04. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocane, mirungi, kubelink
05. Kupigana au kupiga, kutukana au kutukanana na mtu/mwanafunzi yeyoteyule
06. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
07. Kudharau Bendera ya Taifa au/na Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Shule.
08. Kuoa au kuolewa au kuwekwa kimada
09. Kumpa mimba msichana, kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje yashule.
10. Kutoamimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au/na watu
12. Kukataa adhabu kwamakusudi.
13. **Mwanafunzi kuwa na simu yamkononi na vifaa vingine vyovyote vya umeme**
14. kuwepo nje ya shule muda wowote ule wa shule bila kibali cha kumruhusu kutoka nje (kutoroka)

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MPWAPWA

A. Mimi mwanafunzi……..(majina matatu) wa anwani S. L.P..... nimesoma maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari Mpwapwa pamoja na Sheria na Kanuni zake. Nimeelewa vema nami naahidi kuwa mtiifu na mwaminifu wakati wote nitakapokuwa shuleni na mahali pengine popote. Nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu wote na kwa Juhudi na uthabiti nitajifunza kwa bidii ili nipate elimu bora. Nitakuwa mfano mzuri wa kuigwa kwa ajili ya maendeleo yangu,ya shule na Taifa zima kwa jumla.

Sahihi…….. Tarehe:……/...../2022

B. Mimi ..... Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi: …….nimesoma maagizo ya kujiunga na Shule ya Sekondari Mpwapwa pamoja na sheria na kanuni za shule. Naahidi nitamsaidia mwanafunzi huyu kwa hali na mali ili aweze kukamilisha masomo yake ya sekondari bila kipingamizi chochote.

Na nipo tayari kufikishwa kwenye vyombo vya dola endapo nitashindwa kumtimizia kijana wangu mahitaji yake ya msingi yaliyoorodheshwa kwenye. Barua ya kujiunga na Kidato cha Tano. Na maandishi haya yatumike kama ushahidi dhidi yangu.

Nitashirikiana na Uongozi wa Shule ili kutimiza azma hii. Kama sitapatikana tafadhali wafuatao (ndugu watatu) waitwe shuleni pakitokea tatizo au kitu kingine chochote kitakachohitaji uwepo wangu.

i……. Namba ya simu ....Uhusiano wake na
mwanafunzi (**kaka, dada, shangazi, mjomba, shemeji**)……

ii…….. Namba ya Simu ……
Uhusiano wake na mwanafunzi (**kaka, dada, shangazi, mjomba, sheme**ji)……

iii…….....Namba ya Simu .....Uhusiano wake na mwanafunzi (**kaka, dada, shangazi, mjomba, sheme**ji) ……

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MPWAPWA DISTRICT COUNCIL

MEDICAL EXAMINATION FORM

TO THE MEDICAL OFFICER:

NAME OF STUDENT:……..…….....…SEX…….AGE……..

MEDICAL HISTORY

	YES	NO
Tuberculosis		
Asthma		
Heart disease		
Jaundice		
Peptic ulcers		
Epilepsy		
Diabetes mellitus		
Kidney problem		
Anaemia		
Neurosis		

PHYSICAL EXAMINATION: Respiratory system - Cardiovascular system Gastrointestinal system - Urinary system - Reproductive system - Eye: R: - L: - E.N.T-

INVESTIGATION

1. Blood -HB……
   -WBC…….
   -ESR……
   -VDRL Test……
2. Urine – Pregnancy……..
   -Sed……
   -Stool……..

I have examined the above student and considered that he/she is physically and mentally fit/ not physically and mentally fit for further studies.

Name: .....

Signature ;……Date;……

Station; ……

Designation.....

ORODHA YA VITABU KIDATO CHA TANO 2022

GENERAL STUDIES

- Joannes Bigirwamungu & Sospeter; “Understanding General Studies”, 2018
- Nyambari Nyangwine. “General Studies for form 5 & 6”, New syllabus approach, 2009
- Zist Kamili,“General Studies for Advance level”.

PHYSICS

- S. Chand’s, (Class XI, “Principles of Physics”.
- S. Chand’s, (Class XII, “Principles of Physics”.
- Thom Duncan, “A-Level Physics”.

CHEMISTRY

- TIE, (2019), “General Chemistry for Advanced Level Secondary Student’s Book Form Five and Six”.
- TIE, (2019) “Inorganic Chemistry for Advanced Level Secondary School Student’s Book form Five and Six”.
- TIE, (2019) “Physical Chemistry for Advanced level Secondary School Students Book Form Five and Six”.
- TIE, 2019), Organic Chemistry for Advanced level Secondary School Students Book Form Five and Six”.
- S. Chand (I & II), “Conceptual Chemistry”.

ADVANCED MATHEMATICS

- Septine Inyas Silem, “Advanced Mathematics for Secondary School”.
- “Understanding mathematics”.
- “Chandi 1 and chandi 2(A level)”.
- “Pure Mathematics One”.
- “Pure Mathematics Two”.

(Anunue Kitabu kimojawapo)

BASIC APPLIED MATHEMATICS

- Septine I. Sillem, (2014),”Basic Applied mathematics for Advanced Secondary School form VI Student’s Book”.
- Septine I. Sillem, 2nd Edition, (2017) ”Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary School Student’s Book form V”.

BIOLOGY

- "Biological Science (Bsc)"
- "Principle & Application in Biology"
- "Understanding to Biology (UB)"
- "Chand of Biology"

HiSTORY 1

- Salehe Yasin, (2018), "Themes in African History Paper 1".
- Jeannes Bigirwamungu & George Tumaini, (2011), "Understanding African History-History Paper 1 Notes-Advanced Level Secondary School Education Form Five & Six, Afroplus Industries-Dar es Salaam-Tanzania.
- Comrade Shibitali, "Contemporary Historical events- History paper 1".

HiSTORY 2

- Salehe Yasin, "Essential in Advanced level History Paper 2".
- Kato A, "Mastering in Advanced level History Paper 2".
- Zisti Kamili, "History 2 Alive".
- Comrade Shibitali, "Contemporary Historical events- History paper 2".

ENGLISH LANGUAGE 1

- Advanced level English Language 1 (Reviewed Students Class notes)-kinapatikana kwenye Duka la shule.
- "Advanced level English Language 01" by Nicholous Asheli.
- "Advanced level English Language 01"-Oxford
- Advanced Learner's Dictionary.

ENGLISH LANGUAGE 2

- Ashel N,(2010), "Appreciation of Literary work".
- "Stylistic and Communication in English".

LIST OF READINGS

PLAYS

- *Betrayal in the city - Francis Imbuga*
- *I will Mary when I want -Ngugi wa Thiong'o and Ngungi wa Mini*
- *The Bride - Austin Bukenya*
- *Lwanda Magere – Okoiti Omtatah*
- *Black Mamba - John Ruganda*

NOVEL AND SHORT STORIES

- *Encounters from Africa - Macmillan Education Limited*

- *The Beautiful ones not yet Born - Ayi kwei Armah*
- *Divine providence - Severin N. Ndunguru*
- *A man of the people – Chinua Achebe*
- *The rape of the pearl - Magala Nyago*
- *Varnishing shadows - Namige Kayondo*
- *His Excellency the Head of the State – Danny Sajo*
- *A season of waiting - David Omowale*

POETRY

- *Selected Poems - Institute of Education*
- *The Wonderful surgeon and other Poems – Charles Mloka*

KISWAHILI 1

- TET, (2019), "Kiswahili Shule za Sekondari-Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita".
- Jubeck A. Masebo & Nyambari M. Nyangwine, (2016), "Nadharia ya Lugha Kiswahili 1-Kidato cha Tano na Sita".Dar es Salaam-Tanzania.

KISWAHILI 2

- Nyambari Nyangwine"Nadharia ya Fasihi Kidato cha Tano na Sita".

USHAIRI

- *Kimbunga - Haji Gora*
- *Mapenzi Bora – Shaban Robert*
- *Chungu Tamu - Theobald A. Mvungi*
- *Fungate ya Uhuru- Mohamed S. Khatibu*

RIWAYA

- *Usiku Utakapokwishwa - Mbunda Msokile*
- *Kufikirika - Shaban Robert*
- *Mfadhili - Hussein Tuwa*
- *Vuta N'kuvute – Shafi A. Shafi*

TAMTHILIYA

- *Kwenye Ukingo wa Thim - Ebrahim Hussein*
- *Morani - Emmanuel Mboga*
- *Kivuli Kinaishi - Said Mohamed*
- *Nguzo Mama - Penina Muhando*

GEOGRAPHY 1

1. Practical Geography:

- Advanced level PRACTICAL GEOGRAPHY FORM 5 & 6; Map reading & Interpretation' Photography interpretation, Surveying, statistics and research – James Egino Kinunda and Michael Bunyinyiga (2017)

- The essentials of practical Geography, Advanced Level form 5 & 6 (2005)

2. Physical Geography:

- A comprehensive approach to physical geography for secondary schools (Revised Edition), 2019 – DT MSABILA
- Physical Geography for Secondary Schools (2016) – Zist Kamili

GEOGRAPHY 2

- Richard White, (2007) **"African in Focus"** Macmillan Africa-Malaysia.
- Msabila D.T, (2004), **"Human and Economic Geography"** Nyambali Nyangwine-Tanzania.

PHYSICAL EDUCATION

- "Socker science"-Tony Strwdwick
- "Track and field coaching"-Will Freeman
- "Kinetic Anatomic"-Robert Rehnke
- "Applied Sport Mechanics"-Brenda Bwrkett